**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA**

NAMBA ZA SIMU
Mkuu wa shule 0754332325
Makamu wa shule 0752400610
Mwalimu mlezi 0752054579

SHULE YA SEKONDARI
ILEMBO
S.L.P 1731
MBEYA

TAREHE 12/04/2024

Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi
…………………………………………………………..
S.L.P …………………

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILEMBO KIDATO CHA TANO ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA, MKOA WA MBEYA MWAKA 2024 / 2025

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **2024/ 2025**tahasusi ya …………………………….. shule ya Sekondari Ilembo (bweni) ipo umbali wa kilometa 60 kusini mwa Halmashauri ya Mbeya. Wanaotokea njia ya Iringa au Tukuyu washukie stendi ya Nanenane hapo watapanda daladala za Mbalizi. Pia wanaotokea njia ya Tunduma au Mkwajuni (Chunya) washukie stendi ya Mbalizi. Hapo Mbalizi wataulizia stendi ya Umalila watapata mabasi ya kuja Ilembo High School.

Muhula wa masomo kidato cha tano 2024/2025 utaanza tarehe 01/07/2024 kama ilivyotangazwa na TAMISEMI. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2024

### MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### SARE ZA SHULE

i. Sare ya shule hii ni suruali 2. (rangi ya ugoro na zambarau estimu 1) mshono wa mifuko ya pembeni, rinda mbili upande wa mbele na turnup mkunjo wa chini (suruali isiwe modo)

ii. Shati nyeupe mikono mirefu, Tai iendane na kitambaa cha suruali

iii. Masweta yalingane na rangi ya vitambaa vya suruali hapo juu

iv. Viatu ni rangi nyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, soksi jozi mbili nyeusi.

v. Sare za michezo kwa shule hii ni track suit (dark blue)

vi. Nguo ya kushindia ni suruali za khaki na shati ya light bluRRDe

vii. Rangi ya kitambaa cha sare ya shule kimeambatanishwa

viii. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi wa kawaida **MICHANGO MBALIMBALI**

**Weka michango mbalimbali kwenye akaunti ifuatayo**

Jina la akaunti: **Ilembo Secondary School**
Namba ya Akaunti: **61001200174**
Benki: **NMB**

**NB: Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay in Slip.**

**Michango hiyo ni kama ifuatavyo**

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA NI**

(i) Ream (**A4)** za karatasi mbili (2) kwa mwaka.

(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

(iii) Scientific calculator

(iv) Godoro kwa mwanafunzi wa bweni futi 2 na nusu

(v) Mashuka pair 2, blanket 1, foronya 1, chandarua (mashuka, foronya, chandarua ni light blue)

(vi) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko nakikombe)

(vii) Ndoo mbili kubwa 1 na ndogo 1 zenye mifuniko

(viii) Jembe moja lenye mpini lililonolewa, kwanja/sickle iliyonolewa spring file 1, moper 1, na fagio 1 (chelewa)

(ix) Jacket/sweta au koti litakalovaliwa baada ya masomo kujihifadhi na baridi

(x)Mzazi anashauriwa kumtafutia motto wake vitabu kwa matumizi yake binafsi (xi)Nguo za ndani za kutosha

**Orodha ya vitabu muhimu kwa kila somo ni kama ifuatavyo;**

## 1.GENERAL STUDIES

(i) General studies for Advanced Level Certificate, form six (6) by Richard R.F. Mbalase (2011)

(ii) General studies for Advanced Level Certificate, form five (5) by Richard R.F. Mbalase (2011)

(iii) Contemporary approach for advanced level "General Studies Notes" form 5 & 6 by Nyambari C.M. Nyangwine, Godfrey Rutta Nyangwine, Steven O. Maluka (New Syllabus (2009)

## 2. HISTORY

(i) Major issues in African history by Tanzania institute of education
(ii) History of modern Europe by peacock
(iii) How Europe Underdeveloped Africa by W. Rodney
(iv) History in Focus: Modern World History By Ben Walsh
(v) Mastering Advanced Level History Book Two, By Kato, A (2011)
(vi) Mastering Advanced Level History Book One, By Kato, A (2012)

## 3. GEOGRAPHY

(i) Principles of Physical Geography by Monk house (2008)
(ii) Landforms in Africa by Collin Peacock
(iii) Statistics simplified by N. A. Saleem
(iv) Map reading by Mac master
(v) Human and Economic Geography by C.Morgan (1982)
(vi) Map reading, General publications ltd – DSM by Durra, S.E. (2003)
(vii)Geography, an integrated approach, fourth edition by david Waugh (2009) (viii) Practical geography for Africa b fohn m. Pritchard (1990) (ix) R.B. Bunnet (2007) General Geography in diagrams.

## 4. ENGLISH

(i) Macmillan education ltd 2000, encounters from Africa, macmillan
(ii) Ayi Kwei Amah, 1996, the beautiful ones are not yet born, EAEP
(iii) Chinua Achebe, 1991, a man of the people, BAEP
(iv) Ndunguru 1999, Divine providence, Mkuki na Nyota
(v) Magala Nyago, 1985, the rape of the peal Macmillan
(vi) Namige Kayondo, 1995 vanishing shadow, Macmillan
(vii) Danny Sato, 1983, his Excellency the head of state, Macmillan
(viii)David Omowale, 2002, a season of welting, EAEP
(ix) Francis Lubuga, 1990, Betrayel in the city, Heinemann

(x) Ngugi wa Thion'go, et al 1982, I will marry when I want,Eaep
(xi) Bukenya, 1984, the bride, EAEP
(xii) Okot Omitah 1991, lwanda Magere Heinemann
(xiii) Henrik Ibsen, 1974, an enemy of the people, Eyre Matheuen
(xiv) John Rugand 2005, Black Mamba, EAEP
(xv) Charles Mloka, 2002, the wonderful surgeon and other poems, Mkuki na Nyota
(xvi) Tanzania Institute of Education, 1996, selected poems, print pak (T) limited
(xvii) The real English textbook for Advance Level, Dr. Kadeghe Michael

## 5. MATHEMATICS

(i) Scientific calculators
(ii) Basic and Applied Mathematics by Respicius Kiiza (2010)
(iii) Mathematics for class xi & xii by DASS, H.K. & VERMA, R. (2000)
(iv) Pure mathematics (Revised edition) By M.F. Macrae (2011)
(v) Pure mathematics volume 1& 2 by Backhouse, J.K. (1985)
(vi) Core mathematics for Advanced Level by L.Bostock
(vii) Advanced Level Mathematics by L.K. Shayo
(viii) Advanced Level Mathematics vol. I & II by Kinunda (1974)

## 6. ECONOMICS

(i) Principles of economics 4th edition by M.L. Jhighari
(ii) An introduction to modern economic 4th edition by P.Hardwick
(iii) Economics alive I & II by Z. Kamili 2014
(iv) Modern Economics by R. Mudida 2003
(v) Economics a student guide 1992 by Beard Han.
(vi) Introduction to Economics theory 1992 by B.C. Gupta

**Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba; xii. Kusababisha mimba;

xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule LINUS PIUS NYEMBELE**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOTAJWA HAPO JUU -**

**VIAMBATANISHO MUHIMU KWENYE HII FOMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali; ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Uthibitisho wa uraia wa Tanzania kama hana cheti cha kuzaliwa

v. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tahadhari soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**SAINI YA MKUU WA SHULE ……………………….. JINA**

**LA MKUU WA SHULE: LINUS PIUS NYEMBELE**

**MHURI WA MKUU WA SHULE.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OOF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**

ILEMBO SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 1731,
**MBEYA.**

DATE………………………

MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL P.O.BOX
……………………….……………

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please…………………………………………………………… (Student) as to her fitness For pursuing further education at this school

**……………..……………**

**HEADMASTER**

1. Haemoglobin……………………………………………………….
2. P.V. bleeding…………………………………………………………..
3. Blood pressure…………………………………………………….
4. Blood group……………………………………………………….
5. (a) Sight…………………………………………………………………
   (b)Hearing…………………………………………………………….
6. Urine for sugar and pregnancy test………………………………………….
7. Stool for routine-examination……………………………………………..
8. Athma…………………………………………………………………….. 9. Skin diseases…………………………………………………………… 10. Epilepsy………………………………………………………..
11. Leprosy…………………………………………………………..
12. Pulmonary tuberculosis………………………………………………….
13. Deformity…………………………………………………………… 14. Mental problems……………………………………………………..
15. V.D (give type)……………………………………………………………
16. Any other serious disease not mentioned above…………………………………..

………………………………………………………………………………………

OTHER COMMENTS: ……………………………………………………………..

……………………………………………………………

**DESIGNATION AND SIGNATURE**………………………………………

Sahihi ……………………………………………………………………………

Tarehe …………………………………………………………………………..

**WIZARA YA ELIMU, TEKNOLOGIA NA MAFUNZO YA UFUNDI**

**SHULE YA SEKONDARI ILEMBO**

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili ……………………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa………………………………………….. (tarehe, mwezi, mwaka)

3. Kabila……………………………………… Taifa ………………………..

4. Dini na madhehebu ………………………………..……………………………..

5. Jina la Baba ………………………..…………………………………..………………

(namba ya simu )…… ………….…………………………….

6. kazi ya Baba ……… ……………………………………………………………..

7. Jina la Mama………………………………………………………………………………
kazi yake…………………………… namba ya simu …………………………………..

8. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana……………………………………………

10. (a) Jina la mlezi aliyeko mkoa wa mbeya…………………………………………….

(b) Kama ni mlezio uhusiano wako nayeye…………………………………………………

(c) Anwani ya mlezi…………………………………………………………………..………
namba ya simu ………………………………………………..

11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani? (Taja sehemu moja tu utakayo kwenda kila wakati.

(anwani)………………………………………………………………..

12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa ni za kweli na sahihi.

Sahihi ya mwanafunzi…………………………………………… tarehe………………………..

Sahihi ya Mzazi /Mlezi…………………………………………… tarehe……………………….

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAISI**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI Z AMITAA (TAMISEMI) SHULE YA SEKONDARI ILEMBO FOMU YA KIBALI:**

## 1. SEHEMU YA KWANZA

Mimi ……………………………………………………….. ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha TANO mwaka…………………….. katika shule ya Sekondari Ilembo na nitafika shuleni bila kuchelewa. ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za Nchi nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi ya elimu ya kujitegemea.

Anwani yangu ya kudumu ni

……………………………………………

……………………………………………

…………………………………………..

## 2. SEHEMU YA MZAZI / MLEZI:

Mimi ……………………………..………………………………… ninakubali mototo wangu ………………………………………………………………. kuchukua nafasi

kuingia shule ya Sekondari Ilembo ………………………………………… kidato cha TANO mwaka …………………………………………. ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.

Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu kwa shule na Taifa. anwani yangu ya kudumu ni:

………………………………………

……………………………………….

.

…………………………………………

Simu Na.

……………………………………..

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi.

OFISI YA MKUU WA MKOA,

MKOA WA ……………………..,

WILAYA YA ………………………..,

S.L.P ………………………………..

MKUU WA WILAYA,

………………………………………… ……………………………………………….

…………………………………………………..

## UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA

Nathibitisha kuwa …………………………………………………………………. (jina kamili la Mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/ kwa kuandikishwa.

Baba yake (jina kamili)………………………………………………………………..

Amezaliwa katika mkoa wa ………………………………………… wilaya ya …………………

Tarafa ya……………………………………….. kata ya…………………………………….

Mama yake (jina kamili)……………………………………………………………….….

Amezaliwa katika kata ya …………………………………. wilaya ya…………..……………

Mkoa wa ………………………………………………………………………..

**………………………………………..**

**MKUU WA WILAYA**

**NB: MWANAFUNZI KAMA HANA CHETI CHA KUZALIWA NI LAZIMA FOMU HII IJAZWE KWA MKUU WA WILAY HUSIKA AU NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA KIWASILISHWE SHULENI BADALA YA FOMU HII.**